

Changanua msimbo wa QR au tembelea discountedfares.alleghenycounty.us.



Pata punguzo la 50% kwa nauli zako za usafiri leo kwa kutumia Allegheny Go!

Je, unapokea msaada wa SNAP kwa sasa? Pata punguzo la 50% kwa nauli za usafiri kwa mabasi, reli ndogo na huduma nyingine za PRT kwa kutumia Allegheny Go! Allegheny Go kwa sasa inapatikana kwenye programu ya Ready2Ride kwenye kifaa chako cha mkononi na itapatikana kwenye kadi halisi katika mwaka wa 2025.

Je, ninastahiki kwa Allegheny Go?

Washiriki wanaostahiki:

- Wanaoishi katika Kaunti ya Allegheny hivi sasa
- Walio na umri wa miaka kati ya 12 na 64
- Ambao wamekuwa wakipokea misaada ya Mpango wa Usaidizi wa Lishe (SNAP) kwa angalau miezi 3. Hii inajumuisha wewe au mwanafamilia.
- Walio na kifaa cha mkononi na wanaoweza kufikia programu ya Ready2Ride

Je, nitajisajili vipi kwa Allegheny Go?

Ni rahisi. Unaweza kujisajili na kusajili wanafamilia wanaostahiki katika programu moja kwa hatua chache rahisi:

1. Pakua programu ya Ready2Ride na ufungue akaunti.
2. Tembelea discountedfares.alleghenycounty.us ili utume ombi la Allegheny Go.
3. Baada ya kutuma ombi, utapata punguzo lako kwenye programu yako ya simu ndani ya saa 24.
4. Nunua nauli za usafiri zilizopunguzwa bei! Utapata punguzo la 50% kwa kadi ya usafiri ya saa 3, kadi za usafiri za kila wiki, na kadi ya usafiri ya kila mwezi ya siku 31.



 **allegheny go**

Huduma ya Kaunti ya Allegheny
Idara ya Huduma kwa Wanadamu